OUKA
Osaka University Knowledge Archive

Title	Utendaji wa Uganga wa Pepo Zanzibar
Author(s)	Haji, Hassan Gora
Citation	スワヒリ＆アフリカ研究. 27 P.37-P.52
Issue Date	2016
Text Version	publisher
URL	https://doi.org/10.18910/71115
DOI	10.18910/71115
rights	
Note	

Osaka University Knowledge Archive : OUKA

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

Osaka University

Utendaji wa Uganga wa Pepo Zanzibar

Hassan Gora HAJI

0. Ikisiri

Makala haya yanahusu Uganga wa Pepo kama unavyofanywa katika vijiji vya Chaani, Kiwengwa, Mkwajuni na Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini, Unguja, Zanzibar. Makala haya yanatokana na utafiti nilioufanya mwaka 2011, 2014 na 2015.

Katika makala haya mafupi tutagusia uganga wa pepo unavyofanywa, ambao mara nyingi unapofanywa huambatana na nyimbo na muziki. Muziki huo huwa ama wa ala au makofi au viwale unaohusika. Aidha tutazungumzia hatua za uganga wa pepo pamoja na nyimbo zake, ngoma za uganga wa pepo pamoja na aina na majina ya pepo.

1. Utangulizi

Miongoni mwa jadi za Waswahili wa mwambao wa Afrika Mashariki ni imani ya kuwepo majini/pepo, mashetani, vibwengo/bwengo na mizimu. Majini ni wingi wa jini. Jini ni kiumbe dhahania asiyeonekana, aliyeumbwa kwa moto (BAKIZA 2010: 133). Kiumbe huyu ana uwezo wa kuwadhuru binadamu kwa kuwasababishia maradhi mbalimbali kama kichaa, kutozaa na homa ya muda mrefu. Jini pia hutambulika kwa jina la pepo. Shetani ni kiumbe anayeaminiwa kuwa yuko asiyeonekana, aliyeasi na kufukuzwa kwenye eneo la majini (BAKIZA 2010: 364). Inaaminika katika Zanzibar kuwa shetani siku zote ni kiumbe mbaya anayedhuru watu; hakuna shetani mzuri kama walivyo majini. Majini wapo wazuri na wabaya kwa matendo yao kama walivyo binadamu: wako wazuri na wabaya pia. Vibwengo au watu wengine huwaita bwengo. Umoja wake ni kibwengo. Huyu ni kiumbe mdogo ambaye wakati mwingine huonekana na binadamu kwa macho lakini si sana kudhuru watu. Hata hivyo, baadhi ya waganga huwatumia viumbe hawa kuwadhuru watu. Katika (BAKIZA 2010: 157) tunaambiwa kuwa kibwengo ni shetani mtundu asiyedhuru watu. Mizimu ni wingi wa mzimu. Huyu ni aina ya shetani ambaye hutumiwa kuwatatulia watu matatizo yao mbalimbali wanapoombwa kufanya hivyo. Kwa Zanzibar, viumbe hivi hujengewa vibanda (nyumba ndogo sana) au huhifadhiwa katika mapango yam

awe au ya miti mikubwa. Watu wanapokuwa na shida huenda sehemu hizo kuomba au wengine husema kutambika.

Baadhi ya watu wa Zanzibar wanaamini kuwa nguvu na uwezo wa viumbe hao upo katika kulinda mashamba, mali, miji, mitaa, viambo na watu wenyewe. Aidha, viumbe hao huwasibu/huwadhuru binadamu (Alpers 1984: 683) na husaidia kutibu baadhi ya maradhi yanayowasakili binadamu ambayo mengine husababishwa nao. Viumbe hawa, wakati mwingine hutumiwa kusaidia kubainisha dawa zinazohitajika kwa mgonjwa. Itikadi au imani hizi zina nafasi kubwa katika upwa wote wa Waswahili na kwengineko Afrika. Pamoja nazo, Waswahili wana mila zao kama vile ya miiko mbalimbali ambayo hufungamanishwa na imani za ushetani au pepo (Mbaabu, 1985). Kwa mfano: i) ukila gizani utakula na shetani, ii) ukila kiwimawima njiani, au ukienda chooni gizani utakumbwa na shetani na iii) ukikaa kwenye kizingiti cha mlango utapigwa kumbo/defra na shetani. Itikadi hizi, kwa hakika zina umuhimu wake – kuwaasa wanajamii wasifanye mambo ambayo yana madhara kwao. Ukila gizani utakula na shetani ina maana kuwa kula gizani ni hatari kwa sababu huoni; unaweza kula mdudu au kula mwiba na ukakulea madhara. Au ukienda chooni gizani utakumbwa na shetani, ina maana kuwa chooni ni sehemu chafu, unaweza kutereza na kuanguka na pengine uumie. Hata hivyo, Waswahili wanaamini kuwa chooni ni sehemu wanazopenda kukaa shetani wabaya kama makata na makaniki. Kwa hivyo, ukienda giza atakudhuru. Ama kukaa kizingitini si jambo zuri kwani, hapo ni njiani, ukikaa watu wengine hawataweza kupita au wakipita wanaweza kukusukuma na kuanguka na ukaumia, ndio maana tunaambiwa tukikaa kizingitini tutapigwa kumbo na shetani.

Kim (2010) kwa upande wake anaeleza kuwa Waswahili hutafuta msaada wa tiba kwa waganga ambao hutibu maradhi mengi yanayosababishwa na jini na hali hii ya kuwepo jini au shetani huchukuliwa kama ni sehemu ya utamaduni wa Waswahili. Uganga wa pepo au wengine huuita uganga wa shetani ni miongoni mwa mila za kale za Waswahili wa Zanzibar. Uganga wa pepo ni taasisi hai ya tiba ya asili ambapo mgonjwa, baada ya kuchunguzwa kwa ramli au kuonekana dalili za ushetani au upepo, hupewa dawa za mitishamba ili aondokane na ugonjwa alio nao. Lakini ikishindikana mgonjwa kupona kwa dawa tu, huamuliwa kupungwa. Kupungwa ni kuitwa shetani/pepo ili aje kichwani mwa mgonjwa. Baada ya pepo kuja na kutoa salaamu na jina lake kama ilivyo ada, huhitaji alipwe vitu ili ampe afueni mgonjwa. Mara nyingi vitu anavyohitaji ni pamoja na chano, mbuzi, kuku, pete, njiwa na kilemba. Baada ya kukabidhiwa vitu hivyo, mgonjwa hupata uzima na kama ilikuwa hazai, huzaa.

Watu wengi wa visiwa vya Unguja na Pemba (Zanzibar) wanaamini kuwepo pepo na kwamba pepo hao wana uwezo wa kuwadhuru watu, pia. Imani hii ndiyo inasababisha kuwepo uganga wa pepo ambao hufanywa ili kumuondoa pepo anayesababisha madhara kwa binadamu. Uganga wa pepo ni kazi ya kuponya au kutibu wagonjwa ambao wamesibiwa/wamedhuriwa na pepo au shetani kwa kutumia uganga wa sihiri, kisomo, hirizi, kafara[1)] na mitishamba. Katika kufanya hivyo, mganga wa pepo mara nyingine hutumia nyimbo ambazo mara nyingine huambatana na ngoma (Nkwera ht.) na (Fujii 2011). Naye Sengo (1995) anaeleza tu kuwa katika unyago na jando la Waswahili wari huimbiwa nyimbo kama ni sehemu ya dawa kuombewa wapone haraka. Anasema hivi:

"Katika unyago na jando hufanyiwa uganga na wari huimbiwa nyimbo kama dawa, pia" (uk. 129). Anachokieleza Sengo hapa ni kuwa nyimbo za unyago na jando hutumika kama dawa kwa kuimbiwa wari wawapo katika taasisi hizi za kijadi. Lakini nionavyo, nyimbo hizo hazitumiki kama dawa bali kwa lengo la kuliwaza na kufunza *wari* juu ya maisha ya kila siku katika jamii inayohusika.

Mtu ambaye hufanya uganga huu wa pepo hujulikana kwa majina tafautitafauti katika jamii za watu wa Zanzibar na kwengineko duniani. Kwa mfano, watu wa Kaskazini, Unguja humwita kwa majina tafauti kama vile fundi au mganga pia Alpers (1984: 686) analibainsha hili katika makala yake au huitwa mwalimu/maalim au siku hizi hutumika pia jina la ustadhi. Kwa Wazulu wa Afrika ya Kusini, wao mganga humuita Sangoma na wingi wake ni Isisangoma. Sangoma ni istilahi ya Kizulu ambayo kwa huko Afrika ya Kusini sasa inatumika kwa maana ya waganga wote wa kijadi. Kwa Wa-xhosa hujulikana kwa jina la ixwele au amaquira. Kwa Wavenda wao humwita mungome na kwa Wa-tsonga hujilikana kwa jina la n'anga au mungoma.

Maalumati (data) ya kazi hii yamepatikana kwa kutumia mbinu za umakinifu (ushuhudiaji) na mahojiano ya ana kwa ana ambapo mtafiti alipata nafasi ya kuhudhuria shughuli mbalimbali za uganga wa pepo pamoja na kufanya mahojiano na waganga na wari waliowahi kupungwa.

2. Pepo Anavyopatikana na Dalili Zake

Pepo au shetani anaweza kupatikanwa na binadamu kwa kurithiwa kutoka kwa mtu aliyekuwa naye, kumpenda mtu, kumkumba mtu yeyote atakayepita nyumbani kwake au anaweza kutumwa na mchawi kwenda kumdhuru mtu.

[1)] Kafara ni uchawi unaofanywa kwa ajili ya kubadilisha marogo (BAKIZA 2010: 139)

Pepo au shetani hujionesha kwamba yumo katika mwili wa binadamu kupitia ama maradhi ya mwili au akili au kuchanganyikiwa (Giles 1987). Maradhi hayo ni kama vile kupiga kelele ovyoovyo, kushitukashituka usingizini, kupandisha mzuka, kuharibu mimba mara kwa mara, homa za mara kwa mara zisizosikia dawa za hospitali. Na wakati mwengine mwanamke aliyeolewa kutopata mtoto kwa muda mrefu baada ya kuolewa hata kama anapata siku zake na anakutana na mumewe.

2.1 Aina na Majina ya Pepo

Pepo wapo wa aina nyingi na wana majina yao. Kwa mfano, Mwana-wa-Mwana, Simba, Kalibi Kasi, Mwajuma Kirobo, Fungua Lango, Funga Nangwe, Mapara, Mpaji Kani, Ame Mkuwi, Chacha Nangwe, Mkozingo, Fundi Yuni, Gora Kipepo (Mahojiano na Gora na Ussi 2014). Majina haya ya pepo yaliyotajwa yanapatikana Kaskazini, Unguja na hasa katika kisiwa cha Tumbatu. Na aina nyingine ni pamoja na Kitimiri, Nyange, Mrewa (Alpers 1984: 684). Majina haya yanapatikana katika mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Kwa hakika kila kijiji au kiambo huwa na pepo au shetani ambaye huwa anajulikana sana na wanakijiji kinachohusika. Kwa mfano, katika kijiji cha Chaani Kikongeni kuna pepo anayeitwa Kome. Maskani yake ni mtoni. Kwa hivyo, hapo zamani watu walikatazwa kupita au kwenda kufua au kukoga mtoni saa sita za mchana au usiku wa manane. Ukienda nyakati hizo utadhuriwa na shetani huyu. Na kupona kwako mpaka upungwe. Katika kijiji cha Gamba Majenzi kulikuwa na pepo anayeitwa Zuwena. Inasemekana Zuwena alikuwa akionekana mara kwa mara na watu katika umbo la binadamu. Katika kiambo cha Kichungwani, Chaani Masingini alikuwepo mama mmoja ambaye alisibiwa na Zuwena kwa hivyo alikuwa akiumwa mara kwa mara mpaka alipopungwa na Zuwena kujitambulisha kama ni yeye ndiye aliyemdhuru. Baada ya yule mama kupoa, alibeba mimba na alipozaa mtoto wake wa kike alimwita jina la yule pepo yaani Zuwena kwani, ndivyo walivyokubaliana siku ile alipopungwa. Na huyo Zuwena (mtu) hadi leo yupo. Katika kijiji cha Potoa, Kijikweni kulikuwa (tunasema ‘kulikuwa’ kwa sababu siku hizi hatajwi sana) na pepo anayeitwa Kijumsi ambaye maskani yake kwenye mbuyu. Wazee wa Potoa walisema kuwa Kijumsi alikuwa akionekana kwa umbo la binadamu, mwanamke mzuri mwenye nywele ndefu, na alikuwa na kawaida ya kukaa chini ya mbuyu akashana nywele zake wakati wa mchana.

Aidha aina za shetani au pepo, kama watu wengine wanavyowaita, ziko nyingi kama vile pepo wa tari (Alpers 1984) na mara nyingi, aina za pepo/shetani hufungamana na aina ya ngoma ya kupungia

pepo. Kwa hivyo, tunapata aina za pepo/shetani kama vile pepo wa komero (ruhani/pepo mweupe), pepo wa puuo (pepo mweusi), pepo wa mchanja, pepo wa kibuki, pepo wa kibuhudadi, pepo wa kibundi, pepo wa burudai, pepo wa umundi, pepo wa kumbwaya, pepo wa rubamba (pepo wa kichawi) na pepo wa pungwa. Hata hivyo, aina zote za pepo/shetani zimegawika katika makundi mawili makuu: i) pepo wazuri na ii) pepo wabaya. Giles (1987), anasema kuna pepo au majini wa aina mbili: waislamu na washenzi (wabaya) lakini pia shetani au jini au pepo anaweza kuwa muislamu (mzuri/mwema) na mshenzi (mbaya) kama walivyo binadamu, kuna wema na wabaya pia. Pepo wazuri hutumiwa kuwalinda na kuwasaidia watu katika maisha yao ya kila siku na wale wabaya ndiwo wanaowadhuru watu. Mawazo haya pia yanaungwa mkono na Alpers (1984: 687).

Katika kufanya uganga, ili kumtibu mgonjwa aliyesibiwa na pepo, fundi au mwalimu au mganga wa pepo (Giles 1987: 7), mara nyingi hutumia nyimbo ambazo mara nyingine huambatana na ngoma (Nkwera, ht). Mganga hutumia nyimbo kumwita pepo aje kichwani mwa mgonjwa kisha aseme naye na kama yeye ndiye anayemdhuru mgonjwa wapatane ili amuachie/ampe afueni.

Sifa hii ya nyimbo za ugnaga wa pepo, ya kuambatana na muziki kama tulivyoeleza kabla, inaelezwa pia na Rashid (2005) pale asemapo:

> "Wimbo (wa Kiswahili) ni ushairi ambao unaimbwa au kughanwa kwa kufuatanishwa na muziki wa ala/vyombo au mdomo" (uk. 63).

Kwa hakika, wimbo wa uganga unapoimbwa huambatana na muziki. Muziki huo unaweza kuwa ama wa ala/vyombo vya muziki au viwale au sauti za mdomo au kofi au njuga au vishindo vya miguu.

2.2 Hatua za Uganga wa Pepo

Uganga wa pepo katika Zanzibar una hatua mbalimbali katika kuufanya.Hatua hizi ni kwa Zanzibar nzima lakini kwa uganga wa pepo wa maruhani na puuwo. Hatua hizo ni pamoja na:

- Kupiga nyungu
- Kutabana.
- Kuongowa
- Kuwekwa utangani
- Kutoa salamu na jina

- Kulipwa/kupewa chano kidogo
- Kulipwa chano kikubwa
    - Mbuzi/ng'ombe
    - Uzari/Kilemba
    - Pete
    - Kifimbo
- Kuhongera (kufurahia) na kuaga

Kila hatua katika uganga wa pepo ina nyimbo zake isipokuwa katika kutabana.

2.2.1 Kupiga Nyungu

Kupiga nyungu ni kumfukiza mgonjwa wa pepo/shetani kwa kutumia mvuke wa madawa ya mitishamba iliyochemshwa. Nyungu ni aina ya dawa ya mvuke ambao hutengenezwa kwa mchanganyiko wa majani na miti ya aina saba. Miti hiyo hutafautiana kati ya mganga na mganga au baina ya aina moja ya uganga wa pepo na nyingine. Kwa mfano, miti inayotumika katika kutengeneza nyungu ya pepo wa maruhani ni pamoja na mchaichai, mrehani, mdimu, kivumbasi, muudiudi, muwakikali na mkarafuu pamoja na viungo vyake-mpompio, mpachori na marashi ili inukie zaidi. Lengo la nyungu ni kumvuta pepo ili aje haraka wakati atakapoitwa.

Wakati wa kupiga nyungu mwari, katika uganga wa maruhani huimbwa nyimbo kama hizi:

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili Sanifu**
i. Njoo mwana wa jini wee Njoo mwana wa jini wee, tule mnemo.	Njoo mtoto wa jini wee Njoo mtoto wa jini wee, tule ngoma

Katika uganga wa puuwo (uganga wa shetani wa kichawi au pepo mbaya) wimbo kama huu ufuatao huimbwa ili kumueleza mgonjwa ajivukize ili apoe.

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili Sanifu**
ii. Poya wee mwari wangu poya, nami n'pole.	Poa wee mwari wangu poa, na mimi nipoe.

2.2.2 Kutabana

Neno kutabana ni neno la Kitumbatu lenye maana ya kuwarehemu wazee kwa Kiswahili Sanifu. Kabla ya kuanza uganga mwalimu/mganga huanza kwa kuwatakia rehema wazee na kuwaombea dua ili kazi ya uganga iwe rahisi na iende vizuri kwa salama na amani. Katika hatua hii hakuna wimbo wowote unaoimbwa kwa aina zote za uganga, isipokuwa kuomba duwa tu.

2.2.3 Kuongowa

Kuongowa ni kutaja majina ya pepo wakubwa na kuwaita. Baada ya kuwatakia rehema na kuwaombea duwa wazee, kama uganga wa maruhani mganga huanza kwa kusoma Kur-an kisha huendelea kwa kuwataja majini mbalimbali na sehemu wanakokaa na kuwataka waje pale ugangani wasaidie kazi iwe rahisi. Kila baada ya kutajwa majina ya majini au pepo kadhaa, wari waliopungwa zamani na watu wenye mganjwa huitikia kwa kusema:

Sheulila[12)] we e eeeh, mwana wa jini sheulila.

2.2.4 Kumwita Pepo/Shetani

Kabla ya kuanza kumwita pepo, mwari/muwele huletwa utangani na kuwekwa kitako juu ya jamvi au mkeka, tayari kwa kuitwa pepo. Utangani ni sehemu ya kufanyia uganga, inaweza kuwa ndani ya nyumba ya mganga au nje ya nyumba.

Katika hatua za kumwita pepo/shetani na kuwekwa utangani katika uganga wa maruhani nyimbo kama hizi huimbwa:

Wimbo	**Tafsiri - Kiswahili sanifu**
Ijilisu, ijilisu, fili makyani, Salia Manga ee kaumu ruhani.	Kaeni, kaeni, katika masikanini, Mubakie Manga ee jamii ruhani

2) Sheulila au wengine husema sheilila. Neno hili linatokana na maneno mawili ya Kiarabu: Sheikh na Lillah, yenye maana ya Sheikh wa Mwenyenzi Mungu. Lakini katika muktadha wa kiganga neno hili linatumika kumuomba pepo asifanye/aache tabia fulani.

Katika hatua ya mwanzo ya kumwita pepo katika uganga wa puuwo huimbwa wimbo kama huu ili kuwaomba radhi watu wote waliohudhuria uganga kama kutatokea makosa wasamehewe na kama kuna mganga mwengine naye anaombwa ashiriki katika kufanikisha uganga.

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili sanifu**
Taireni eee, taireni waganga Tunangia kiringeni, Taireni waganga.	Tunakuombeni radhi, tunakuombeni radhi waganga Tunaingia ugangani (pahala panapofanyiwa uganga) Tunakuombeni radhi waganga

2.2.5 Kuja pepo/Shetani

Baada ya pepo kuja kichwani mwa muwele, watu hufurahi na wimbo kama huu wa rubamba huimbwa kuonesha furaha yao na hiyo furaha hufananishwa na utamu wa sukari.

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili sanifu**
Mwari wenu keshafika zamani, jamaa we, Uno si utamu sukari, Mwari wenu keshafika zamani, Uno si utamu sukari. Kibungu na Marekani jini we, Mwenyefaidi dola nini? Nani, nani? Mwenyefaidi dola nani? Mwari wenu keshafika zamani, Uno si utamu sukari.	Mwari wenu ameshafika zamani, jamaa we, Huu si utamu sukari, Mwari wenu ameshafika zamani, Huu si utamu sukari, Kibungu na Marekani jini we, Anayefaidi dola nani? Nani, nani? Anayefaidi dola nani? Mwari wenu ameshafika zamani, Huu si utamu sukari

2.2.6 Kutoa Salaamu na Kutaja Jina

Katika hatua ya kutoa salamu na kutaja jina nyimbo kama hizi katika uganga wa maruhani huimbwa:

i. Nipatie langu kombe

   Nitoe salaamu nende zangu.

ii. Kilio hum, furaha jina

   Kilio hum, furaha jina.

Katika uganga wa puuwo (uganga wa shetani wa kichawi), wimbo kama huu ufuatao huimbwa ili kumjuvya pepo kuwa akishakuja ni sharti ajitambulishe kwa kutoa salaamu kwa watu wote waliohudhuria katika shughuli ya uganga.

Jini weee, jini akija hutoa salaamu,
Walaina aaaah wasalaamu, salaamu x3.

Kwa kawaida salaamu hutolewa mara tatu (Asalaam alaikum) kisha yule pepo hutaja jina lake, kwa mfano, husema: jinni, wa jinani, wa kahatani. Ikiwa anasisita kutoa salaamu huimbwa wimbo kama huu katika uganga wa maruhani ili kumfahamisha kuwa salaamu hutolewa mara tatu:

Unipe salaamu we, unipe salaamu wee
Unipe salaamu nyengine,
Kaningoje jabalini, usinune,
Unipe salaamu nyengine.

Hata hivyo, ikiwa pepo anachelewa kuja kichwani kwa muwele/mwari kuna nyimbo kama hizi huimbwa ili kushajihisha pepo aje haraka, asichelewe. Wimbo huu ni wimbo wa uganga wa puuo. Hapa pepo huulizwa kwa nini anachelewa kuja. Naye hujaaliwa kuwa anachelewa kuja kwa sababu anawasubiri watoto wake ili waje pamoja.

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili sanifu**
Hunakuja kunangoja nini bwengo wee? Nangoja wanangu wee ee x2 Wenda Mrima, Eeeh, wanangu, wee Wenda Mrima.	Huji unangojea nini kibwengo wee? Nangojea watoto wangu wee ee x2 Waliokwenda Mrima, Eeeh, watoto wangu, wee Waliokwenda Mrima

Ama katika uganga wa maruhani wimbo kama huu ufuatao huimbwa ili kumuharakisha pepo aje haraka kwa sababu waganga wamechoka kupiga ngoma na kuimba:

Njoo mwana wa jini we,

Tumechoka kinganga mkononi,

Njoo mwana wa jini.

2.2.7 Kupewa Chano Kidogo

Chano ni jumla ya vyakula ambavyo hupewa pepo baada ya kuitwa na kusemeshwa na kupatana na wenye mgonjwa. Hii ni kama ada ya pepo, akiitwa kwa mara ya mwanzo na akishakuja hutaka apewe vyakula, yaani chano. Vyakula vinavyofanya chano ni pamoja na mkate wa mchele, haluwa, tende, muwa mweupe au mweusi, sukari guru, zabibu, sharubati, yungiyungi jeupe au bluu na ndizi mbivu ya pukusa. Vyakula hivi vikiwa vichache na mkete mdogo ndio huitwa chano kidogo. Baada ya chano kuletwa utangani, wari wa zamani (waliopungwa zamani) ndio huanza kula na baadaye muwele hulishwa.

Katika hatua ya kupewa chano kuna nyimbo ambazo huimbwa. Kwa mfano, wimbo huu ufuatao huimbwa wakati chano kinaletwa utangani kwa ajili ya kukabidhiwa muwele na kuliwa. Wimbo huu unazungumzia kuwa chano kinacholetwa ni cha babu na watoto lakini hakina hakijapambwa lakini mtu akikosa kitu kimoja hutafuta kingine.

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili sanifu**
Kino chano cha Babu, waride Mbona hakina zuwaride, zuwaride, Mwenye landa hugombea msumeno, Naukwereze.	Hiki chano cha Babu, watoto Mbona hakina mapambo, mapambo, Mwenye landa hutaka msumeno, Naukwereze

Wakati wa kuliwa chano wimbo kama huu huimbwa hasa katika uganga wa maruhani. Katika wimbo huu tunafahamishwa kuwa mtu hupokea kitu anachopewa na kwamba hicho huwa ndio chake na ndicho hupaswa kukitumia:

Mkono we mkono, pokea upewacho,

Usichopewa ujuwe si chako, mkono

Jini we utoke wende zako.

2.2.8 Kupewa Chano Kikubwa

Chano kikubwa ina maana kuwa mwari/muwele hupewa chano cha vyakula na mbuzi, kilemba pamoja na kileso, njiwa manga (mweupe kwa maruhani au mweusi kwa jinni mweusi/mbaya), pete na /au fimbo ya mpingo. Vitu hivi ama hutolewa kwa pamoja au kwa awamu, inategemea uwezo wa mgonjwa na walivyokubaliana na pepo.

2.2.9 Kupewa Uzari (Kilemba)

Katika hatua ya kupewa *uzari* (kilemba) pia kuna nyimbo zake kama hizi zifuatayo:

i. Maruhani pima kilemba chako.
Maruhani,
Pima kilemba chako.

Kilemba ni kitambaa cheupe (kwa maruhani na cheusi kwa pepo wa rumbamba au puuo) cha aina ya bafta chenye urefu wa mita mbili na nusu au mita tatu. Kabla ya kukabidhiwa kwanza hukamatwa na wanaume wenye nguvu ncha na ncha kisha wari waliopungwa zamani huanza kukipima kwa kukishika kutoka upande mmoja hadi mwengine huku wakiimba na kucheza. Baada ya kupimwa, kilemba hukunjwa urefuurefu na kushikwa katikati na mwari wa zamani ambaye ameshapewa kilemba na kisha humgusiaha sehemu moja moja kuanzia kichwani hadi miguuni. Wakati huu wimbo unaofuata hapa chini huimbwa. Baada ya hapo, mwari huvishwa kilemba chake na kucheza nacho.

ii. Pima kilemba we, pima kilemba we,
Mbiombio.

2.2.10 Kupewa Mbuzi

Katika hatua ya kupewa/kulipwa mbuzi katika uganga wa maruhanii huimbwa wimbo kama huu unaofuata hapa chini. Wimbo huu huimbwa ili kuonesha furaha ya kukabidhiwa mbuzi aliyemtaka.

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili sanifu**
Nachungia ng'ombe nachungia x2, Somalo, fumo na ngao, nachungia ng'ombe ijayo.	Nafurahia ng'ombe nafurahia x2 Somalo, mkuki na ngao, Nafurahia ng'ombe ajae.

2.2.11 Kupewa Pete

Katika hatua/wakati wa kupewa pete katika uganga wa maruhani kama komero wimbo kama huu huimbwa. Pete anayokabidhiwa inakuwa ya fedha au dhahabu, inategemea pepo alivyotaka au uwezo wa muwele. Wimbo huu unaofuata hapa chini unaeleza kuwa Mkozingo (jini) alipopita kwa Mwana wa Mwana (jini) alibisha hodi lakini Mwana wa Mwana hakutaka kuitikia/kumkaribisha jinni mwenzake, Mkozingo lakini hata hivyo akamuambia Harija (jini mwengine waende hivyohivyo wakamvishe pete mtoto/jini aliyekuwa bado hajapewa pete kwani ilikuwa ni furaha kubwa kwao kukabidhiwa pete mwenziwao).

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili sanifu**
Mkozingo nipopita kwa Mwana, nikapiga hodi seitikiwa Harija twende we, twende Jide, Tukamvishe pete mtoto. Danda we horia, danda we. Horia, Danda.	Mkozingo nilipopita kwa Mwana nikapiga hodi sikuitikiwa, Harija twende we, twende Jiddah, Tukamvishe pete mtoto Ng'ara we horia, ng'ara we Horia, Danda

2.2.12 Kupewa Njiwa Manga

Pepo wote (wa maruhani, wa puuo au wa rubamba) hupewa njiwa manga ikiwa alihitaji pale alipoitwa. Jini au pepo wa maruhani hupewa njiwa mweupe tititi na pepo wa rubamba au puuo hupewa njiwa mweusi tititi. Njiwa hatakiwi kuwa na rangirangi. Akiwa na rangi zaidi ya moja atakataliwa na italazimu kutafutwa njiwa mwengine ama siku ileile au siku nyingine watakayokubaliana.

Katika hatua ya kupewa njiwa katika uganga wa pepo wa maruhani huimbwa wimbo kama huu ufuatao. Wimbo huu unaeleza kuwa huyo jini apewe njiwa manga ili afurahi, katika kufurahi huko atakuwa akipanda na kushuka jabali. Hapa limetajwa jabali kwa sababu katika imani za Waswahili ni kuwa jini hukaa katika majabali makubwa kama nyumba zao.

Nipatie njiwa manga mweupe

Nipande jabali niteremke.

2.2.13 Kupewa Fimbo/Rungu

Katika hatua hii ya kupewa fimbo kama ni jumla ya mapambo ya pepo/jini nyimbo kama hii ya uganga wa maruhani huimbwa na kwamba jini wa maruhani hupewa fimbo kama silaha ya kujilinda na maadui wake. Lakini jini wa rubamba, yeye hupewa rungu kwani, rungu ndiyo inayotumika kuuliya watu uchawini, inavyoaminika. Wimbo kama huu huimbwa katika uganga wa rubamba au wa puuo:

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili sanifu**
Bi kirembo rungu ishalengwa, Haijalengwa, haijalengwa, Ikilengwa hutambuya mwenyewe inapokwenda we.	Bi Kirembo rungu imesharembewa, Haijarembewa, haijarembewa, Ikirembewa hutambua mwenyewe inapokwenda.

Katika kuonesha furaha ya kukabidhiwa fimbo, katika uganga wa maruhani, wimbo kama huu huimbwa. Unapoimbwa wimbo huu wachezaji hucheza kwa kurukaruka na fimbo zao huku wakizigonganisha juu huku wakipishana kutoka upande mmoja kuelekea upande mwengine na kukutana katikati.

Kimanga we kimanga,

Mwacheni aruke kimanga,

Shurushuru,

Mmanga kwa upanga

Shurushuru,

Mmanga kwa upanga.

2.2.14 Kuhongera

Kabla ya kumaliza uganga kuna hatua ya kuhongera (kufurahi) baada ya pepo kupanda kichwani mwa muwele nyimbo kama hizi huimbwa:

Miye we miye,

Majini husema miye,

Nipe ulilonitia,

Majini husema miye.

2.2.15 Kumaliza/ kuaga

Katika hatua ya kumaliza uganga au kuaga, kwa mfano, katika uganga wa rubamba au puuo nyimbo kama hizi huimbwa, wimbo huu huimbwa ili kumfahamisha mwenye mgonjwa kuwa kazi aliyowapa waganga imekamilika, wanahitaji ujira wao ili waende zao.

Wimbo	**Tafsiri – Kiswahili sanifu**
Mwenye kazi kazi yako isha njoo ukagule Uje utupe kinuwa mgongo uje utunule.	Mwenye kazi kazi yako imekwisha njoo ukague, Uje utupe kinua mgongo uje utuinue

Kwa jumla, uganga wa pepo au shetani huambatanishwa na nyimbo, ngoma na uchezaji. Mara nyingi nyimbo hizo huimbwa na mganga mwenyewe, mwari au muwele; na jamaa wa mgonjwa pamoja na waalikwa.

3. Hitimisho

Kutokana na data tulizozichambua katika makala haya tumebaini kuwa waswahili wa Zanzibar wana mila ya kuamini uwepo wa pepo au shatani ambao wana uwezo wa kuwadhuru binadamu. Aidha wanaamini kuwa dawa ya watu waliosibiwa na pepo ni kupungwa yaani, kufanyiwa uganga wa pepo. Katika kufanya uganga wa pepo/shetani, Wazanzibari, kama tulivyoona katika vijiji vya Chaani, Kiwengwa, Mkwajuni na Tumbatu vilioko katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na kama ilivyojitokeza katika uganga wa puuwo na maruhani kuwa uganga ulifanywa kwa kufuata taratibu na hatua mbalimbali. Katika kufanya uganga huo kulikuwa na hatua za kupiga nyungu, kutabana/kuwarehemu wazee, kuongowa, kumwita pepo, kuja pepo, kutoa salamu na kutaja jina, kupewa chano, kuhongera na kuaga. Kuna vyano vya aina mbili kuu: chano kidogo na chano kikubwa. Chano hutolewa kwa kufuata utaratibu maalumu. Kwanza hutangulia chano kidogo kisha chano kikubwa. Katika kula chano pia kuna utaratibu wake. Wanaoanza kula chano ni wari wa zamani ambao tayari wameshapewa chano kisha hulishwa mwari mpungwa. Hatua zote katika kufanya uganga zinaweza kufanywa siku moja au siku mbalimbali kutengemea nafasi ya mganga na /au uwezo watu wa mgonjwa. Lakini mara nyingi hufanywa katika siku mbalimbali. Pia tulibaini kuwa ili pepo apewe chano kama vyakula tu, au kilemba, au mbuzi ni sharti kwanza aitwe na baada ya kuitwa na kuja kichwani atoe salamu na ataje jina lake na

/au maskani yake. Kama hakufanya hivyo hakuweza kupewa chano chake. Baada ya kutimizwa hayo ndipo mgonjwa hupata nafuu au hupona maradhi yake.

Aidha katika makala haya tulibaini kuwa katika kila hatua wakati wa kufanya uganga wa pepo, ispokuwa katika hatua ya kuwarehemu wazee, kulikuwa na muziki na nyimbo ambazo ziliimbwa kufuatana na dhima za hatua hizo za uganga zinazohusika. Kwa mfano, katika hatua ya kutoa salamu na kutaja jina, wimbo kama huu huimbwa ili kusisitiza na kumuomba pepo kupitia mwari mpungwa kutoa salamu zaidi ya mara moja kama ndio ada wala asikasirika.

Unipe salaamu we, unipe salaamu wee
Unipe salaamu nyengine,
Kaningoje jabalini, usinune

Kwa hakika kila kijiji cha Zanzibar kina mganga au waganga wa pepo na kila mganga ana namna yake ya kufanya uganga. Wapo wanaotibu kwa kusoma Kur-an tu, wengine Kur-an pamoja na dawa za mitishamba na wengine hupunga/huganga kwa kupiga muziki na kuimba nyimbo. Nyimbo hizi za uganga wa pepo, kama zilivyo nyimbo simulizi nyingine, hurithiwa na kila mmoja akatumia madoido yake katika uimbaji. Nyimbo hizi za uganga wa pepo ni fupi sana. Kwa hivyo, hulazimu kurudiwarudiwa mara nyingi wakati wa kuimbwa. Kutokana na namna nyimbo hizi zinavyorudiwarudiwa huwezi kutabiri mwisho wa wimbo unaoimbwa. Mwisho wa wimbo unaoimbwa huamuliwa na mwimbaji mwenyewe anapotaka.

Uganga wa pepo kwa Zanzibar haufanywi kwa siri; hasa ule unaoambatana na nyimbo na ngoma/muziki. Wakati mwingine hufanywa ndani ya nyumba maalum iliteuliwa kwa kazi hiyo. Na aghalabu huwa nyumba ya mganga au hufanywa nje, hadharani, usiku au mchana, inatengemea uamuzi wa mganga.

Mwisho, napenda kutoa maoni yangu kuwa uganga wa pepo katika Zanzibar uko a aina nyingi. Kuna uganga wa rumbamba, kabuki, koikoi, kubwaya, umundi, kitari na nyinginezo. Kwa hakika aina hizi nyingine hazijafanyiwa utafiti kwa hivyo, ni vyema watafiti wengine wangefanya utafiti katika eneo hili ili kuzielewa vyema imani na mila za Waswahili na kulinda na kuhifadhi amali hizi.

Marejeo

Alpers, E. A. 1984 "Ordinary Household Chores: Ritual and Power in a 19TH –Century Swahili Women's Spirit Possession Cult". *The International Journal of African Historical Studies*, 17 (4). pp 683- 687.

Fujii, C. 2011. "Comparative Studies of the Medicine of the Sunna and Uganga". *Kyoto Bulletin of Islamic Area Studies*, 4-1&2, 2011. Pp156-189.

Giles, L. 1987. "Possession Cults on the Swahili Coast: A Re-Examination of Theories of Marginality". *Africa*, 57 (2). pp 240-241.

Kim, C.C. 2010. 'Jinn Possession and Uganga (Healing) among the Swahili: A Phenomenological Exploration of Swahili Experiences of Jinn'. *Christian Muslim Encounter*, 3 (2). pg 69

Mbaabu, I. 1985. *Utamaduni wa Waswahili.* Nairobi: Kenya Publishing & Book Marketing Co.Ltd.

Nkwera, F. V. (h.t.). *Tamrini za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: Business Printers Limited.

Rashid, A. M. 2008. "Namna ya Kutunga Bahari Mbalimbali za Ushairi wa Kiswahili." ~~Katika~~ *Utamaduni wa Mzanzibari* . uk. 63-67. Zanzibar: BAKIZA.

Sengo, T. S. Y._1995. "Itikadi za Waswahili." Mlacha, S. A. K. na Hurskaini, A. (wahariri.) *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Uk.37-43. Dar es Salaam: TUKI and Helsinki: DAAS.

Ancestral Wisdom. Sangoma

http://www.ancestralwisdom.com/sangoma.html.

(Imedurusiwa tarehe 5 Julai, 2014; 10: 20 pm.)

Gateway Africa. Traditional African Herbal Medicines

http://www.gateway-africa.com/gateway-africa/tradmedicine/index.html.

(Imedurusiwa tarehe 5 Julai, 2014; 10: 35 pm.)